TANGAZO LA SERIKALI NA. 512 la tarehe 21/05/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA VIBALI VYA SHUGHULI ZA BURUDANI NA SHEREHE YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Shughuli za Burudani na Sherehe za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni a Mwaka, 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri

ya Manispaa ya Kinondoni au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"shughuli ya burudani" maana yake ni shughuli yoyote halali inayojumuisha sherehe, michezo na muziki.

Maombi ya kibali

4.-(1) Mtu anayekusudia kufanya shughuli ya burudani au sherehe katika eneo la Halmashauri anapaswa kuwa na kibali cha maandishi kilichotolewa na Halmashauri.

(2) Maombi yote ya vibali yataambatana na malipo ya ada kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Utaratibu wa kuomba kibali

5.-(1) Mtu anayekusudia kufanya shughuli ya burudani au sherehe katika eneo la Halmashauri anapaswa kuomba kibali kwa Mkurugenzi kupitia kwa Afisa Utamaduni husika kwa kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yataeleza jina la mwombaji, aina ya burudani au sherehe, tarehe, muda wa kuanza na kumalizika kwa burudani au sherehe na eneo husika.

(3) Endapo maombi ya kibali yatakataliwa, Halmashauri itamtaarifu mwombaji kwa maandishi na kueleza sababu za kukataliwa kwa maombi hayo.

(4) Endapo Halmashauri imetoa kibali na ikadhihirika kuwa kuna sababu za msingi za kuzuiliwa kwa shughuli husika kabla au baada ya kuanza kwa shughuli hiyo, Halmashauri itamtaarifu mwombaji kwa maandishi na kueleza sababu za kuzuiliwa kwa shughuli hiyo.

(5) Nakala ya kibali kilichotolewa itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi Wilaya ikiwa na kiambatanisho cha stakabadhi ya malipo ya ada.

Wajibu wa mmiliki wa ukumbi

6. Mmiliki wa ukumbi wa muziki, burudani au baa anatakiwa-

(a) kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha desibo hamsini na tano kuanzia saa sita mchana hadi saa nne usiku na desibo arobaini na tano kuanzia saa nne usiku hadi saa kumi na mbili asubuhi;

(b) kuonesha picha mjongeo au sinema kwa sauti ya chini kiasi cha desibo hamsini na tano kuanzia saa sita mchana hadi saa nne usiku na desibo arobaini na tano kuanzia saa nne usiku hadi saa kumi na mbili asubuhi; na

(c) kuhakikisha mwanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane haingii katika ukumbi na iwapo itabainika kuingia kwa mwanafunzi au mtoto hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Vigezo vya utoaji kibali

7. Halmashauri itatoa kibali iwapo itajiridhisha na mambo yafuatayo:

(a) shughuli ya burudani au sherehe inayoombewa kibali haitasababisha uvunjifu wa amani;

(b) eneo linaloombewa kibali cha kufanyia shughuli ya burudani au sherehe linaruhusiwa kwa shughuli inayoombewa kibali;

(c) kumbi za burudani au sherehe zina usalama wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa vifaa vya kuzima moto, madirisha makubwa ya kuingiza hewa, milango inayofunguka kwa urahisi wakati wa dharura; na

(d) shughuli ya burudani au sherehe haikiuki maadili ya kitanzania.

Katazo

8.-(1) Mtu hataruhusiwa-

(a) kumruhusu mwanafunzi au mtu yeyote aliye

Sura ya 13

chini ya umri wa miaka 18 kuingia kwenye sehemu ya starehe au muziki baada ya muda ulioruhusiwa kuisha au kulingana na Sheria ya Mtoto ; au

(b) kuonesha picha mjongeo ambazo hazina maadili katika ukumbi wa picha mjongeo , snema au sehemu nyingine yoyote.

(2) Endapo mwanafunzi au mtu chini ya umri wa miaka 18 atakutwa katika eneo la starehe au muziki, mwanafunzi au mtu huyo, mzazi au mlezi na mtu anayehusika na sehemu hiyo ya starehe au muziki watawajibika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Muda wa kuonesha sinema au picha mjongeo

9.-(1) Muda wa kuonesha sinema au picha mjongeo utakuwa ni kuanzia saa kumi kamili jioni hadi saa sita kamili usiku kwa siku za kazi.

(2) Kwa siku za Jumamosi na siku za sikukuu, muda wa kuonesha sinema au picha za mjongeo utakuwa ni kuanzia saa saba mchana hadi saa kumi na mbili jioni.

Mamlaka ya kufanya ukaguzi

10.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia mahala popote panapofanyika shughuli ya burudani au anapoamini kuna shughuli ya burudani inafanyika muda wowote kwa lengo la kukagua iwapo shughuli hiyo ina kibali au inafuata masharti ya kibali.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake chini ya kanuni ndogo ya (1), Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo yoyote ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli ya burudani kulingana na hali itakayobainika baada ya ukaguzi kufanyika.

Mkusanyiko wa watoto

11.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kukusanya watoto kwa ajili ya shughuli yoyote ndani ya Halmashauri bila kibali cha maandishi.

(2) Mkusanyiko wowote wa watoto katika viwanja vyovyote vya burudani ulioruhusiwa na Halmashauri kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) utafanyika katika siku za mapumziko na kuanzia saa nne kamili asubuhi na kuamalizika kabla ya saa kumi na mbili jioni.

(3) Mtu aliyepata kibali cha mkusanyiko wa watoto atawajibika kwa usalama wao kipindi chote cha mkusanyiko huo na kuhakikisha wanatawanyika kwa usalama kutoka katika eneo la mkusanyiko.

(4) Mtu mwenye mamlaka juu ya eneo la burudani hataruhusu au kusababisha mkusanyiko usio na kibali cha Halmashauri.

Vibali visivyotozwa ada

12.Mikusanyiko ifuatayo itaombewa vibali bila kulipa ada:

(a) mikusanyiko ya kidini;

(b) misiba na mazishi;

(c) michezo ya watoto isiyotozwa.

Usafi wa mazingira

13.-(1) Mtu yeyote anayeendesha shughuli za burudani ndani ya mamlaka ya Halmashauri atalazimika kufanya usafi ndani au nje ya eneo lililotumika katika shughuli ya burudani kwa kuondoa uchafu wote uliosababishwa na shughuli hiyo ya burudani.

(2) Mtu anayekiuka kanuni ndogo ya (1) atawajibika kulipa gharama ya uchafuzi wa mazingira kadri zitakavyokadiriwa na Halmashauri na gharama zingine ambazo Halmashauri itaingia katika kuondoa uchafu huo.

Muziki unaoleta kero

14. Mmiliki wa leseni ya biashara hataruhusiwi kupiga muziki zaidi ya desibo hamsini na tano kuanzia saa sita mchana hadi saa nne usiku na desibo arobaini na tano kuanzia saa nne usiku hadi saa kumi na mbili asubuhi.

Ukamataji wa vifaa

15.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya

kukamata vifaa vyovyote vitakavyokutwa katika shughuli ya burudani ambayo haina kibali au inaendeshwa bila kuzingatia masharti yaliyoainishwa kwenye kibali husika.

(2) Vifaa vitakavyokamatwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) vitachukuliwa na kuhifadhiwa katika Ofisi za Halmashauri au eneo lolote litakaloamuliwa na Halmashauri.

(3) Vifaa vitakavyokamatwa vitatakiwa kukombolewa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kukamatwa na baada ya hapo Halmashauri inaweza kuuza vifaa hivyo kwa mnada baada ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama.

(4) Mtu yeyote anayetaka kurejeshewa vifaa vilivyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa gharama za ukamataji, usafirishaji na ulinzi wa vifaa hivyo.

Makosa na adhabu

16. Mtu anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kutalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilishaji kosa

17. Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili, endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na kulipa ada anayodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

ADA YA KIBALI

| Namba | Aina ya Shughuli ya Burudani na au Sherehe | Kiwango cha Ada kwa kila onesho au tukio (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Tamasha la Muziki<br>(a) Linalohusisha wasanii wa ndani ya Nchi<br>(b) Linalohusisha wasanii wa nje ya Nchi | (a) 700,000/=<br>(b) 1,000,000/= |
| 2. | Muziki kwenye kumbi za burudani | 50,000/= |
| 3. | Sherehe za mashirika au taasisi mbalimbali | 100,000/= |
| 4. | Onesho la Sinema (isipokuwa maonesho ya kidini) | 50,000/= |
| 5. | Ushereheshaji katika sherehe au tukio | 30,000/= |
| 6. | Picha mnato za tukio | 20,000/= |
| 7. | Maonesho ya sanaa au vichekesho | 50,000/= |
| 8. | Mapambo | 30,000/= |
| 9. | Studio ya kurekodi sanaa | 21,250/= kwa mwaka |
| 10. | Mashindano ya urembo ndani ya Wilaya | 100,000/= |
| 11. | matangazo mtaani kwa kutumia spika (yasiyo ya kidini) | 50,000/= |
| 12. | Kibali cha sherehe za kijamii zinazofanyika ndani ya kumbi. | 100,000/= (ada hii inalipwa na mtu anayefanya sherehe husika na sio mmiliki wa ukumbi). |
| 13 | Sherehe mbalimbali za kijamii ikiwemo harusi, sherehe za kidini na nyinginize zinazofanyika majumbani | 20,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5 (1))*

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI

SEHEMU YA KWANZA
(Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la mwombaji ........................................................... | 2. Anwani ya mwombaji ......................................... |
| 3. Aina ya shughuli ........................................................... | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli ................................................. |
| 5. Muda wa kuanza .......................................................... | 6. Muda wa kumaliza ............................................ |
| 7. Ada ya kibali (Shilingi) ................................................ | 8. Namba ya Stakabadhi ya malipo ........................................... |
| 9. Saini………………………… | 10. Tarehe………………….…..... |

SEHEMU YA PILI
(Kwa Matumizi ya Ofisi tu)

| | |
|---|---|
| 1. Maombi namba .......................... | 2. Ada ya kibali shilingi ................. |
| 3. Namba ya stakabadhi ya malipo .................................................. | 4. Tarehe ya malipo ...................................... |

| | |
|---|---|
| 5. Jina la Afisa aliyepokea malipo .................................................. | 6. Saini ..................................... |
| 7. Muhuri | |

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*futa isiyohusika*)
Sababu: ……………………………..…………………………………………
Jina:………………………………Saini: ……………Tarehe………………..

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ................ya Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Shughuli za Burudani na Sherehe ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, niko tayari kulipa kiasi cha ada ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………
MBELE YANGU:
Jina:…………………………………..……………………
Saini………………………..……………………….………
Wadhifa:…………………………………………………………
Tarehe…………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imegongwa kwenye sheria ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni uliofanyika tarehe 24 mwezi 08 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo mbele ya ;

HANIFA SULEIMAN HAMZA
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni*

SONGORO KHAMISI MNYONGE
*Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
10 Disemba 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais (Tawala za mikoa na serikali za mitaa)*